

OPENER EXAMINATIONS TERM 2 YEAR 2021

KISWAHILI KIDATO CHA TATU

KARATASI YA TATU (FASIHI)

MUDA; SAA 2^{1/2}

JINA.....DARASA.....NAMBARI.....

MAAGIZO: Jibu maswali yote katika karatasi hii

SEHEMU YA A: TAMTHILIA YA KIGOGO

1. “Do! Do! Simameni! Simameni! Leo kutanyesha mawe!

- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)
 - b) Fafanua mbinu za lugha z ilizotumika katika dondoo hili. (al.4)
 - c) Fafanua sifa sita za msemaji. (al.6)
 - d) Eleza umuhimu wa msemaji. (al.2)
 - e) Fafanua maudhui yoyote mawili yanayojitokeza katika dondoo. (al. 4)
- 2.** Fafanua matatizo yoyote kumi yanayowakabili wanasagamoyo. (al.20)

SEHEMU YA B: FASIHI SIMULIZI.

- 3.** a) Eleza umuhimu wa nyimbo katika usimulizi wa hadithi. (al.4)
- b) i) Eleza maana ya misimu. (al.2)
 - ii) Taja mifano yoyote miwili ya misimu. (al.2)
 - c) Taja sifa tatu za vitanza ndimi. (al.3)
 - d) Taja sifa tatu za vitendawili. (al.3)
 - e) Fafanua umuhimu wa vitendawili. (al.6)

4. SEHEMU YA C: USHAIRI.

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yote.

Akosaye shukurani, zako juhudi hajali,
Hata mfanyie nini, haoni huyo hajali,
Hata mpe milioni, matusi ndio stahili,
Aona huna akili, ni yeye ndiye mshindi.

Patia kila la shani, bure unajisumbua,
Takuona kama nyani, tena atakunyambua,
Akuona punguani, chochote hutaambua,
Usingoje shukurani, tenda wema wende zako.

Utafute kwa juhudi, bila kukata tamaa,
Mpe apate faidi, wala asipate njaa,
Hatachoka kukaidi, atakuletea baa,

Na mawazo yakujaa, maishayo hafikiri.

Mpe vyote vya haluwa, wenzako wamtamani,
Hatakupa ya muruwa, juhudi haioni,
Ataka kuzidishiwa, asubuhi na jioni,
Ufanyacho hathamini, aongeze ya karaha.

Si ndugu wala si mwana, si rafiki si jirani,
Shukrani kiwa hana, jua uko hatarini,
Hadharani tatukana, aulize ndiwe nani,
Ambe kama hajaona, kinyangarika kamawe.
Hebu yeye msaili, amepata toa nini?
Haweziye kukubali, kukupa hata thamani,
Ni bure wake ukali, akutia mashakani,
Yake wala hayaoni, mwovu hana shukurani.

Mfadhili watengaje, jana alikuopoa,
Mwaema wambwekeaje, mabaya wayachokoa,
Mzazi wadharauje, mbali alishakutoa,
Sasa jaribu kupoa, ujifunze shukurani.

Maswali

1. Lipe shairi hili anwani mwafaka. (al.1)
 2. Hili ni shairi la aina gani? Thibitisha. (al.2)
 3. Eleza dhamira ya mshairi katika shairi hili. (al. 2)
 4. Bainisha mifano mitatu ya uhuru wa mshairi katika shairi hili. (al.6)
 5. Andika ubeti wan ne kwa lugha nathari. (al. 4)
 6. Taja na utolee mfano tamathali zozote mbili za usemi katika shairi. (al.4)
 7. Eleza maana ya neno hili kama lilivyotumika katika shairi hili. (al1)
- Shani